

## UJENZI WA MIFUMO YA TEHAMA SERIKALINI


“

**M**amlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) yenyekujumu la Kuratibu, Kusimamia na Kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma, imeshirikiana na Taasisi za Umma kuleta mapinduzi katika matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Serikalini. Matumizi hayo yanalenga kuleta ufanisi na kurahisisha utendaji kazi.

e-GA kwa kushirikiana na Taasisi za Umma, imesanifu na kutengenezwa Mifumo mbalimbali ikiwa ni pamoja na *Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG)*, *Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office)*, *Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwateru (HCMIS)*, *Mfumo wa Pamoja wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha (TeSWS)*, *Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Mamlaka ya Maji (MAJIIS)*.

Mifumo mingine ambayo imesanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka kwa lengo la kuongeza ufanisi na kurahisisha utendaji kazi ni *Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS)*, *Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia simu za Mkononi (Government Mobile Platform - mGov)* \*152\*00# (Menyu) & 15200 (SMS), *Mfumo wa Vibali (e-Vibali)* na *Mfumo wa Mikutano kwa Njia ya Mtandao (e-Mikutano)*.

Kaimu Meneja wa Huduma za Ushauri na Uelekezi Bi. Joan Valentine amesema kuwa kazi hizi zinafanya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao ambayo inaitaka e-GA kuwezesha Taasisi za Umma kupata miundombinu na mifumo ya TEHAMA ya pamoja ili kupunguza gharama za uendeshaji Serikalini.



Bi. Joan Valentine  
Kaimu Meneja wa Huduma za Ushauri na Uelekezi

*Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao imetengeneza mfumo wa Ubadiishanaji tarifa unaojulikana kama Government Enterprise Service Bus - GovESB ikiwa ni jitihada za khakikisha Mifumo inabadilishana taarifa*

”

Bi. Joan Valentine  
Kaimu Meneja wa Huduma za Ushauri na Uelekezi

